

Bibilia ya watoto  
Inawalettea

Yoshua  
Achukua  
Madaraka



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Janie Forest  
Alastair P.

Imerekebishwa na: Ruth Klassen

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,  
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya

Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.




Musa alifariki. Yoshua akajua Mungu sasa amemchagua kuongoza Waisraeli. Kabla ya Yoshua kuandaa jeshi lake, alijiandaa kwanza yeye mwenyewe. Mungu alimuahidi Yoshua ushindi na mafanikio katika Nchi ya Ahadi iwapo watu watatii Neno la Mungu wakati wote.



Waisraeli waliahidi kumfuata Yoshua na kutii  
Neno la Mungu wakati wote. Kwa hekima, kiongozi  
mpya alituma wapelelezi katika nchi ya Kanani ili

kuchunguza ulinzi  
wa jiji kubwa  
la Yeriko.  
Iltarajiwa  
kwamba Israeli  
watapigana vita ya  
kwanza ya hapo.






Mtu fulani alimwambia Mfalme wa Yeriko kwamba kulikuwa na wapelelezi mjini. Akatuma askari wake kuwatafuta. Utafutaji ukaanzia kwenye nyumba ya Rahabu ambapo watu hao walikuwa wanakaa. Askari waligonga kwa nguvu kwenye mlango wake. Upesi, Rahabu akawaficha hao watu chini ya mabua ya kitani.




Askari walipoondoka,  
Rahabu akatumia  
kamba nyekundu  
kuwashusha hao watu  
salama nje ya ukuta  
wa mji. Kwa nini  
aliwasaidia  
wapelelezi? Kwa  
sababu alijua Mungu  
alikuwa pamoja nao.  
Alitaka Mungu aokoe  
maisha yake.  
Wapelelezi wakaahidi  
kumuokoa Rahabu na  
familia yake.



Kabla ya kufika Yeriko, Waisraeli walipaswa kuvuka mto Yordani ili kuingia Kanani, nchi ya Ahadi. Lakini hapakuwa na daraja! Watu wangevukaje?





Mungu alimwambia Yoshua kwamba makuhani watawaongoza maaskari na watu, wakibeba sanduku la agano lenye Amri Kumi. Miguu ya makuhani ilipogusa ukingo wa mto, Mungu akatenda muujiza. Mungu akatengeneza njia kavu katikati ya maji.






Baada ya watu wote  
kuvuka mto salama,  
waliweka mawe makubwa  
kumi na mawili katikati ya  
mto na mawe mengine  
kumi na mawili kando ya  
mto upande wa Kanani.  
Mawe hayo yalikuwa kwa  
ajili ya ukumbusho wa  
kuwasaidia watu  
kuwafundisha watoto wao  
kuhusu uwezo na upendo  
mkuu wa Mungu.





Yeriko ilikuwa  
na kuta imara na  
pana sana. Wakati  
Yoshua akipanga jinsi  
ya kushambulia, Mungu  
akatuma Amiri Jeshi  
wa jeshi Lake kutoka  
Mbinguni kumkumbusha  
kiongozi mpya wa  
Israeli kwamba  
Mungu atawashindia  
vita watu Wake.







Mungu alimwambia Yoshua jinsi ya kushambulia Yeriko. Ulikuwa mpango wa ajabu. Watu wa Mungu walitakiwa kuzunguka mji mara moja kila siku kwa muda wa siku sita, na mara saba katika siku ya saba. Kisha walitakiwa kupiga tarumbeta na kupiga kelele, na ndipo kuta za mji zingeanuka chini!



Yoshua na jeshi lake wakafanya kama Mungu alivyoamuru. Labda watu wa Yeriko waliwacheka. Lakini baada ya kuzunguka mara ya saba katika siku ya saba kuhani alipiga tarumbeta ya pembe ya kondoo mume.

Na kama Mungu alivyokuwa ameahidi ... KUTA KUU ZA YERIKO ZIKAANGUKA!





Nyumba ya Rahabu pekee  
iliyokuwa ukutani ikawa salama.  
Aliacha kamba nyekundu ikining'inia  
kwenye dirisha. Mara, watu wa  
Yoshua wakamuokoa Rahabu  
na familia yake. Kisha Yeriko  
ikaharibiwa, kama Mungu alivyoamuru.





Kwa uaminifu, YOSHUA  
akaweka wakfu dhahabu, fedha na  
hazina kwa ajili ya huduma ya Mungu.  
Kisha akatamka laana kwa mtu yeyote  
atakayeujenga tena mji huu mwovu.





Mara kila mtu Kanani  
akasia jinsi Yoshua alivyoshinda  
Yeriko. Wakajua kwamba Mungu  
alikuwa pamoja na watu Wake.



Yoshua Achukua Madaraka

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Yoshua 1-6

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130





Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

